## Ukaguzi wa kiafya ni nini?

### Na unagharimu pesa ngapi?

Ukaguzi wa kiafya unajumuisha maswali kuhusu historia yako ya kiafya, maswali kuhusu chanjo ulizopokea, na ukaguzi wa kimwili. Ukaguzi wa kiafya huenda ukajumuisha kupimwa maradhi yafuatayo:

- Kifua kikuu
- Homa ya manjano ya B
- Homa ya manjano ya C
- Magonjwa ya zinaa
- Kolesteroli
- Anemia na ugonjwa wa sumu ya risasi
- Vimelea
- UKIMWI

Ukaguzi wa kiafya unafaa kufanywa ndani ya siku 90 za kuhamia Washington. Nyingi ya gharama yake italipwa na Washington Apple Health kwa wakimbizi.



## Nyenzo zingine za karibu kwa wakimbizi

**Pierce Transit (Kampuni ya Usafirisha Abiria)**
**piercetransit.org**
*Taarifa kuhusu huduma ya basi, ratiba na nauli.*

**Idara ya Huduma za Kijamii na Afya**
**dshs.wa.gov**
*Msaada wa stempu za chakula, huduma ya watoto, matibabu na pesa taslimu.*

**Nyumba ya Jamii ya Tacoma (Tacoma Community House (TCH))**
**(253) 383-3951 • tacomacommunityhouse.org**
*Usaidizi kwa jamii za wahamaji, kama vile ajira, fursa za elimu, masomo ya lugha, na zaidi.*

**Vituo vya Udhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa (CDC) Afya ya Mhamaji na Mkimbizi**
**cdc.gov/immigrantrefugeehealth**
*Taarifa na takwimu kuhusu afya ya mkimbizi na mhamaji nchini Marekani.*

**Huduma ya Raia wa Marekani na Uhamaji (USCIS)**
**uscis.gov**
*Taarifa kuhusu hali ya Kadi ya Mkazi wa Kudumu, uraia, au sheria za ajira.*

Tacoma-Pierce County
Health Department
*Healthy People in Healthy Communities*

Rev. Sept. 9, 2022

# Mwongozo wa Programu ya Afya kwa Wakimbizi

*Karibu Kaunti ya Pierce, Washington*



Tacoma-Pierce County
Health Department
*Healthy People in Healthy Communities*

**tpchd.org**

## Mbona ninahitaji kufanyiwa ukaguzi wa kiafya?

**Ukaguzi wa kiafya ni moja ya mchakato wako wa kuhamia makazi mapya.**

Ili upate Kadi yako ya Mkazi wa Kudumu ya kisheria (“Kadi ya Kijani” (“Green Card”)), au uende shuleni au chuo kikuu, lazima upokee chanjo zako zote. Ili upokee chanjo hizo lazima kwanza ufanyiwe ukaguzi wa kiafya nchini Marekani.

**Pia, ukaguzi wa kiafya:**

- Utatambua matatizo yoyote ya kiafya yanayokuzuia kufanya kazi
- Utahakikisha umepokea matibabu ya magonjwa yoyote ambayo huenda ukawa nayo
- Utasaidia kukulinda kutokana na maradhi ya kuambukiza

## Ninapanga miadi ya ukaguzi wangu wa kiafya aje?

**Idara ya Afya ya Kaunti ya Tacoma-Pierce (Tacoma-Pierce County Health Department) itampigia daktari wako simu na imueleze kwamba umewasili.**

Ofisi ya daktari itakupigia simu ili upange miadi.

**Ni muhimu sana kwamba usichelewe kwa miadi yako.**



## Ni nini kitafanyika wakati wa ukaguzi huo?

**Daktari atazungumza na wewe na akaungue afya yako.**

Ikihitajika, daktari atakutuma kwa huduma za wataalamu kama vile wa daktari wa meno, macho, kiakili, nk.

**Nchini Marekani una haki mbili muhimu za afya:**

- **Huduma za mkalimani:** Unaweza kuomba mkalimani ili uwasiliane na daktari wako vizuri zaidi.
- **Usiri:** Daktari au muuguzi wako hawezi kufichua jambo lolote linalohusu afya yako kwa mtu yoyote bila ruhusa yako.

## Ninaenda kufanyiwa ukaguzi wa afya wapi?

Kituo cha Matibabu cha Tanbara Mashariki (Eastside Tanbara Medical Center)
Huduma ya Afya kwa Jamii (Community Health Care)
1708 East 44th Street
Tacoma, WA 98404
(253) 471-4553 Mkondo 3210

**Ikiwa ungependa kuwa na mkalimani wakati wa ukaguzi wako, basi kliniki hiyo itahakikisha yupo.**

## Ninafaa kuja na nini kwenye ukaguzi wangu wa kiafya?

**Tafadhali kuja na yafuatayo kwenye ukaguzi wako wa kiafya:**

- Mkoba wako wa Shirika la Kimataifa ya Uhamaji (IOM) pamoja na rekodi zako zote za matibabu na eksirei ya kifua.
- Rekodi zako za chanjo
- Madawa au mitishamba yoyote ambayo unatumia
- Hati za kisheria (kadi ya I-94, pasipoti, nk.)